

Maswali na Majibu kuhusu Mafumbo ndani ya Kanisa Katoliki

By DIN - Melkisedeck Leon Shine · February 16, 2020

Mafundisho ya Katekismus · #Karibu AckySHINE · #Katoliki: Kanisa Katoliki · #Katoliki: Mafumbo ya Imani

Neno hili kuwa nafsi tatu kwa Mungu mmoja laitwaje?

Laitwa fumbo la Utatu Mtakatifu. (Lk, 3:21-22)

Kanisa linafafanua fumbo la umwilisho?

Linatamka kuwa Yesu Kristo ni Mungu kweli na Mtu kweli. (Ebr 4:15)

Nini maana ya neno "Fumbo"?

Fumbo ni ukweli ambao hatuwezi kuelewa kikamilifu, lakini tunasadiki kwa kuwa Mungu hutufumbulia. (Math 11:27)

Katika dini yetu yapo mafumbo hasa mangapi?

Mafumbo matatu

1. Fumbo la Utatu Mtakatifu 2. Fumbo la Mungu Kujifanya mtu 3. Fumbo la Ukombazi wetu

Printable AckySHINE Article · <https://ackyshine.com/post.php?post=988>